



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HB/W:20/22/Vol.V/74

18 Aprili, 2024

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda anawatangazia Watanzania wenyе sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kuomba nafasi ya kazi ya Mkataba wa Miezi Sita (06) iliyotajwa hapo chini.

**1. AFISA UKUZAJI VIUMBE MSAIDIZI KWENYE MAJI DARAJA LA II (AQUACULTURE ASSISTANT GRADE II) - (NAFASI 1).**

**1.1 SIFA ZA MWOMBAJI.**

- Kuajiriwa wenyе mojawapo ya Stahahada katika fani za Ukuzaji Viumbe Kwenye Maji (Aquaculture), Sayansi ya Kwenye Maji na Uhifadhi wa Mazingira (Aquatic Environmental Sciences and Conservation), Sayansi ya Kwenye Maji na Mazingira (Aquatic Sciences and Environment), Elimu ya Viumbe Kwenye Maji (Marine Biology) kutoka vyuo vyovyote vinavyotambuliwa na Serikali.

**1.2 MAJUKUMU YA KAZI.**

- i) Kutekeleza Sheria na Kanuni zinazohusiana na kuendeleza ukuzaji viumbe kwenye maji;
- ii) Kuhimiza Ukuzaji endelevu wanaokuzwa kwenye maji;
- iii) Kuhamasisha njia bora za uvunaji na uhifadhi wa mazao yatokanayo viumbe wanaokuzwa kwenye maji;
- iv) Kuendesha mafunzo ya ukuzaji viumbe kwenye maji;
- v) Kusimamia ukusanyaji, uchambuzi na tafsiri ya takwimu za ukuzaji viumbe kwenye maji;
- vi) Kutafiti au kushiriki katika shughuli za utafiti wa ukuzaji viumbe kwenye maji kadri zitakavyojitokeza katika eneo lake la kazi;
- vii) Kukagua ubora wa mazao yatokanayo na ukuzaji viumbe kwenye maji na kuhakikisha yanakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa;
- viii) Kuhamasisha kuongeza thamani katika mazao yatokanayo viumbe wanaofugwa kwenye maji, ili kuimarisha biashara na Masoko yake;
- ix) Kukusanya maduhuli yanayotokana na mazao ya viumbe wanaokuzwa kwenye maji; na
- x) Kufanya kazi nyininge za fani yake atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

**1.3 MSHAHARA.**

- Mshahara utakuwa ni Tshs. 350,000.00 kwa mwezi.

**2. MASHARTI KWA UJUMLA.**

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenyе umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.

- Vyaombaji wote waambatishe nakaia ya cheti cha kuzaliwa na Kitambulisho cha Uraia (NIDA) au namba ya NIDA kwa ambao hawajapata Kitambulisho.
- Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (Detail CV) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma yaani nakala ya vyeti vya Kidato cha Nne au Sita pamoja na vyeti vya taaluma (Professional Certificate from respective Board, computer certificate) na picha mbili za rangi za hivi karibuni.
- Testmonial, provisional results, Statement of results, hati ya matokeo ya Kidato cha Nne (Form IV) na Kidato cha Sita (Form VI) **havitakubalika kabisa.**
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA na NACTE) na taarifa ya ulinganifu iambatishwe kwenye maombi.
- Waombaji wa nafasi za ajira waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza **tofauti na hapo maombi hayo hayatapokelewa.**
- Kichwa cha barua ya maombi kitaje nafasi ya kada unayoomba kwa ufasaha.
- Barua ya maombi isainiwe na mwombaji mwenyewe tofauti na hivyo maombi hayo **yatakataliwa**
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahuksika watachukuliwa hatua za kisheria.
- Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili kupitia mbao za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, website ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambayo ni [www.bundadc.go.tz](http://www.bundadc.go.tz), namba zao za simu na anuani walizotumia kwenye barua ya maombi ya kazi.
- **Barua zitumwe kwa njia ya Posta au ziwasilishwe kwa mkono masijala ya wazi ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa tisa na nusu (09:30) alasiri.**
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 01 Mei, 2024.
- Maombi yote ya kazi yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
 Halmashauri ya Wilaya ya Bunda,  
 S.L.P 126,  
**BUNDA.**

- Limetolewa na;



Oscar J. Nchemwa

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
 HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA**

---

Barua zote zitumwe kupitia anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P 126, Bunda-Mara, Simu: Namba 028 2621055, Fax Namba: 0282621264, tovuti: [www.bundadc.go.tz](http://www.bundadc.go.tz), Barua Pepe:ded@bundadc.go.tz